

More past papers are available on <http://www.kenyaplex.com>

Kenya Methodist University Ushairi wa Kiswahili(KISW 212) (LSWA 210) (KISW 022) Past Paper

MUDA: SAA MBILI

Maagizo:

Jibu maswali yoyote matatu.

Swali la Kwanza

Fafanua maana ya ushairi

(al. 2)

Eleza tofauti zilizopo kati ya ushairi wa kimapokeo na ushairi wa kisasa.

(al. 18)

Swali la Pili

Taja watunzi watatu waliotunga mashairi yao kabla ya maajilio ya mkoloni.

(al. 3)

Ni maudhui gani yaliyojitokeza zaidi katika mashairi yaliyoandikwa kabla ya wakoloni.

(al. 3)

Jadili mabadiliko ya kimaudhui yaliyojitokeza baada ya ukoloni. (al. 14)

Swali la Tatu

Eleza umuhimu wa ushairi katika jamii.(al. 20)

Swali la Nne

Fafanua dhana zifuatazo za ushairi ukitoa mifano mwafaka.

(al. 10)

Inkisari

Tabdila

Mazida

Kubananga sarufi

Utohozi

Mbali na matumizi ya lugha, kuna vipengele vingine muhimu ambavyo huzingatiwa katika uchambuzi wa mashairi. Fafanua vitano kati ya vipengele hivyo.

(al. 10)

Swali la Tano

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MALI

Kupenda mno ukwasi, naona nitapotea

Mali ina wasiwasi, sikai nikatulia
Mali huzua maasi, mtu yakampotoa
Mali ni njema hidaya, hili kweli najua
Sura yangu iwe mbaya, watu wataisifia
Lakini naona haya, sifa hii kuipokea.
Mali ni nzuri hidaya, tena nikakariria
Lakini ina hekaya, ngumu kuizingatia
Hususa huwa kayaya, dunia kuizamia.
Mali pale niko nayo, wengi wanainamia
Bali nikitokwa nayo, rafiki wanikimbia
Na nipigapo miayo, pembeni wanizomea.
Mwenye mali huzuzuka, kheri akaziambaa
Na heshi kubabaika, kushukushuku jamaa
Na huko kufilisika, akuhofu kila saa.
Umesikia karuni, mali tumzuzua
Mali ilimfitini, dongo likamfukia
Ni khatari yumkini, kwa as-habu rupia
Maadui wa mkwasi, ni wengi kupindukia
Rafikize si halisi, ghalibu humdowea
Wamchomoe fulusi, kisha wamtete pia
Kheri nikidhiwe haja, shida zikinifikia
Nile kadiri ya haja, na nione njaa pia
Na niipate faraja, dhiki zikinitokea
Ee Mola wangu bwana, Jalla wa ala Jalia
Ufukara Maulana, nakuomba nepushie
Nipe riziki mwanana, haja kunitoshelea.
Ukinipa utajiri, nipe na elimu pia
Mali zangu nijajiri, ziwafalie insia
Nakushukuru Qahari, vile kunifadhilia.
Eleza umbo la shairi hili.

(al. 5)

Taja manufaa sita na madhara matatu ya kuwa na mali.

(al.9)

Andika ubeti wa tisa kwa lugha ya nathari.

(al. 3)